**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI MAGOMA

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule**

**0715238352/0743084157**

**Makamu Mkuu wa Shule**

**0715683437/0767463538**

**Patron**

**0756429580/0715830360**

**Shule ya Sekondari Magoma**

**S.L.P 370**

**Korogwe**

**13/6/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGOMA HALMASHAURI YA WILAYA KOROGWE MKOA TANGA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …………..

Shule ya Sekondari MAGOMA ipo umbali wa Kilometa 38 Kaskazini-Mashariki mwa Mji wa KOROGWE Usafiri wa basi kutoka mjini KOROGWE unapatikana katika kituo cha mabasi KILOLE Nauli ni Shilingi 4000 hadi Magoma (Makangara) ,shuka magoma(makangara) kwenda shule chukua pikipiki nauli ni tsh.2000 hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/8/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/8/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/8/2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni kwa Wavulana ni suruali 2 pale green purple

Ili kuepuka mkanganyiko wa rangi ya  suruali zinapatikana shuleni wasiliana na makamu mkuu wa shule.

ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu aje nayo

iii. Sare ya Michezo ni tshirt nyekundu na bukta nyekundu sizizo na maandishi yoyote na raba za michezo
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pea mbili
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta 1 rangi ya dark blue ( zinapatikana karibu na shuleni).
viii. Nguo za kushindia suruali 2 damu ya mzee iwe ndefu chin inch 14 isiwe modo tutaikataa.na t-shirt 2 nyekundu zisizo na maandishi.
ix. Tai 2 rangi ya suruali
x. Tisheti (T-shirt) rangi kijivu (zinapatikana karibu na shuleni.0

Xi Aje na kitambulisho cha bima ya afya NHIF au CHF iliyokatwa ndani ya mkoa wa Tanga.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i)Madaftari 8 quire 4 na ndogo 6 kwa ajili ya test

**ii) Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha hiyo hapo chini)*

1. **HISTORY** –

**(i)** Mastering His tory by Carto pp 1 & 2

**ii)** nyambari nyangwine & stephano maluka –major events in African History P 1

iii).Flourence Mavunde –Basic themes in advanced level History pp2 based on current syllabus

2010).TIE History for advanced secondary school  pp1&2

v).Yasin salehe essential in advanced level history pp 1&2

**2. GEOGRAPHY**

**(i).** Contemporary issue in Geography by Msabila

**(ii)** Intergrated approach Essential of practical Geography Advanced level (Form 5 & 6).

**3.ECONOMICS**

(.i) **AMBROS O.(2018) Essential for A-level Economics pp1& 2**

**(ii) DEWETT K.K.(2005)** Modern economics theories S.CHAO and company LTD pp1&2

**(iii) MWAKAGILE Economics made simple pp 1&2**

iv)AMBILIKILE CM(2012) Economics for Advanced level pp2 and professional studies,Nyambari nyangwine publishers

**4.ADVANCED MATHEMATICS**

**(i).** Bostock, L., Chandler, S. **(1994)** ***The core course for a-level*** **(new edition)**

**(ii)** Dass, H. K. (2010). **Engineering mathematics**

**(iii). Pure Mathematics** 2 by J.K. Bachouse  et al

**(vi) Pure Mathematics 1** by J.K. Bachouse et al

**5. BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM)**

**(i)** Basic applied mathematics ( BAM) for advanced level form 5 &6

**6. GENERAL STUDIES**

**(i)** A level General studies contemporary approach notes F5&6 By Nyambari nyangwine & maluka

ii) General studies Question and answersBased on 2010 sylabas

N.B -VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI SIO MALI YA SHULE ,NUNUA KULINGANA NA TAHASUSI YAKO ,KILA SOMO UNAWEZA KUNUNUA NAKALA MOJA MOJA PP1&2

i. Scientific Calculator;
ii. Uje na godoro upana 2.5 ft
iii. Mashuka Jozi 2 rangi pink na foronya ya godoro 2 pinki, chandarua 1 bue bahari
iv. Nguo za ndani za kutosha;
v. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) silver
vi. Ndoo 2 ndogo na kubwa 1 ( zenye mifuniko;)
vii. Kwanja 1, jembe 1 na mpini, reki 1 na mpini, panga, na mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye akaunt ya shule **41501200067 MAGOMA SECONDARY SCHOOL.** Mwanafunzi aje Bps(karatasi ya malipo original)

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE**

**(B). REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**MAGOMA SECONDARY SCHOOL,**

**P.O.BOX 370,**

**KOROGWE.**

**DATE………………………………**

**MEDICAL OFFICER,**

……………………………………………..GOVERNMENT HOSPITAL.

**NAME OF STUDENT:…………………………………………………………………………………………………………………**

Please examine the above named student to ascertain his/her fitness for further studies.

……………………………………………………………..

**HEAD OF SCHOOL.**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

[To be completed by the medical officer].

I have examined the above named students with regard to:

Skin ……………………………Eyes,………………………Ear………………Chest………..………Eyes …………………………… Spleen ………………… Abdomen …………………… Urine ………………………………………Stool ………………………… Haemoglobin

……………………… Sickle cell ……………………………………………………others………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………………………….

**And I considered.**

1.He/She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias, and fit to go to school.

2.He/Sheisnowtoreturntoschoolhavingtreatmentfor
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
name& signature of medical officer ………………………………………………………………………………………………….

Date: ………………………………………………

**JAZA FOMU HII NYUMBANI KABLA YA KUFIKA SHULENI AU SIKU YA KURIPOTI, UNAPORIPOTI UWE NAYO NA IWE IMEJAZWA TAYARI.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS.**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V)**

**SHULE YA SEKONDARI MAGOMA,**

**S.L.P370,**

**KOROGWE.**

**TAREHE……………………………**

---

**(C).FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA.**

**SEHEMU A**; **Taarifa za mwanafunzi (IJAZWE NA MWANAFUNZI).**

---

1.Jina kamili………………………………………………………………………….…………………………………

2.Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………

3.Wilaya alipozaliwa…………………………………kata……………………………………..kijiji…………………………

4.Kukubali nafasi. ***(Ijazwe na mwanafunzi)***

**Mimi**………………………………………………………………………………………nimesoma na kuelewa maagizo

yote ya Shule ya Sekondari ya Magoma na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule.Nitakapokuwa shuleni Magoma nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

**Sahihi yamwanafunzi………………………………………………………….Tarehe…………………………………….**

**SEHEMU B; Taarifa** za **mzazi/mlezi** (Ijazwe na mzazi /mlezi).

---

1. Jina kamili ………………………………………..…………………………………………………………………
2. Wewe ni Mzazi au Mlezi? (Kata isiyohusika)
3. Kazi yako ……………………………………………………………………………………………………………….
4. Anwani ya mzazi/mlezi **S.L.P**…………… ……………………………………….………… **N.B.** ***NAMBARI YA POSTA IJAZWE KWA AJILI YA KUPOKEA RIPOTI FOMU ZA MWANAO***, jaza anwani sahihi, kama huna tafuta iliyo karibu yako ni muhimu sana.

5. Namba tatu za simu ikiwemo ya mzazi/mlezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi

(a)……………………………….………(b)…………………………………………(c)……………………………………

**UTHIBITISHO**


**M**imi mzazi/mlezi wa…………………………………………………………………………………..………..Nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu **sehemu A hapo juu.**

**Sahihi ya mzazi/mlezi……………………………………………………………………………..**

**Tarehe…………………………………………………………………………………………………….**

**NB. JAZA FOMU HII NYUMBANI KABLA YA KUFIKA SHULENI AU SIKU YA KURIPOTI, UNAPORIPOTI UWE NAYO NA IWE IMEJAZWA TAYARI.**

**KARIBU SANA MAGOMA SEKONDARI**




……………………………………

**MUSTAFA R. MBURI**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0715238352**
- **Makamu Mkuu wa Shu 0715683437/0767683437**
- **Mwandamizi Taaluma 0717314550**
- **Mwandamizi Malez 0715830360/756429580**